

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Mei 18, 2015

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tume kutoa taarifa yake kuhusu tukio la Mtoni Mtongani la Januari 27, 2015

JUMATANO Mei 20, 2015 Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) itakutana na Waandishi wa Habari kuzungumzia taarifa yake ya kiuchunguzi kuhusu tukio lililotokea Januari 27, 2015 huko Mtoni Mtongani, Wilayani Temeke jijini Dar es Salaam, ambapo Jeshi la Polisi lilidaiwa kuwapiga na kuwadhalilisha viongozi na wafuasi wa Chama cha Wananchi (CUF).


Kufuatia tukio hilo Tume ilifanya uchunguzi wake wa kina na kubaini mambo kadhaa na kuyatolea mapendekezo.

Mkutano huo unatarajiwa kufanyika Makao Makuu ya Ofisi za Tume, **Haki House, Mtaa wa Luthuli**, kuanzia **saa 4:00 Asubuhi**.

Tume ilifanya uchunguzi huo kwa mujibu wa mamlaka yake iliyopewa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Sheria Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na.7 ya Mwaka 2001.

Vyombo vyote vya Habari vinakaribishwa kwenye mkutano huo.

Imetolewa na:


Mhe. Bahame Tom Mukrya Nyanduga
Mwenyekiti

Mei 18, 2015